

*Shairi lifuatalo limeandikwa na Aziz Ponary Mlima wa Gothenburg Sweden, likiwa kama Tanzania ya Kifo cha Mzee Abdulrabi Hamisi Muhogo wa Mbeya, Tanzania ambaye alifariki Tarehe 25 Julai 2003, Dar Es Salaam. Katika shairi hili Tunakumbushwa umuhimu wa kushikamana na sala na kumuomba Mwenyezi mungu, kuzingatia elimu, ikiwa kama mkazo wa mawaidha ya Marehemu Hamidu Tambwe, mapenzi baina ya ndugu katika familia.*

## ABDULRABI

### A

1. **A**lifu napiga hodi, mwanafunzi naingia,  
Kuandika imebidi, *Abdulrabi* kusudia,  
Dua kwake sina budi, umbali umezua,  
Peponi pawe ni kwenu, kwa maisha ya daima.

### B

2. **B**uriani babu yetu, kwaheri kwa kutuacha,  
Uchungu sasa ni kwetu, ndugu uliotuacha,  
Simanzi ni mali yetu, kwa jonzi uliloacha  
Peponi pawe ni kwenu, kwa maisha ya daima.

### D

3. **D**ada ulikuwa naye, Hanifa kwa jina lake,  
Kizazi chake wanae, Hamidu kwa uja wake,  
Hakuna afananae, ukarimu jadi yake,  
Peponi pawe ni kwenu, kwa maisha ya daima.

### U

4. **U**rithi wake Hamidu, undugu kuuthamini,  
Na elimu kuimudu, ufunguo duniani  
Ulevi kutosujudu, si fahari maishani  
Peponi pawe ni kwenu, kwa maisha ya daima.

### L

5. **L**aazizi babu zetu, Rajabu, Saidi pia,  
Maghufira nia yetu, Rabana Mola jalia,  
Zipokee duwa zetu, kinabibi kusudia  
Peponi pawe ni kwenu, kwa maisha ya daima.

### R

6. **R**afadha babu karimu, hatamu uliishika,  
Nasaba uliikimu, kwa penzi liloshikika,  
Si sote tulihitimu, kuweza kuja kuzika,  
Peponi pawe ni kwenu, kwa maisha ya daima.

### A

7. **A**zizi Thabiti pia, Meya Rajhoma Machila,  
Tulipo si Tanzania, umbali waleta hila,  
Kuja ilikuwa nia, ghaibu kaziba mila,  
Peponi pawe ni kwenu, kwa maisha ya daima.

### B

8. **B**aragumu limelia, sote tumelisikia,  
Babu katutangulia, njia kututakasia,  
Sala kuzishikilia, pepo kuikusudia,  
Peponi pawe ni kwenu, kwa maisha ya daima.

### I

9. **I**tibari nilikusudia, beti tisa kudondosha  
Deni sijalifukia, kenda nimehitimisha,  
Buriani mlokimbia, safari kuikamilisha,  
Peponi pawe ni kwenu, kwa maisha ya daima.

*Aziz Ponary Mlima  
Gothenburg-Sweden  
July 28th 2003  
19.00 hrs. CET*

---